

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Utangulizi

Tarehe 07 Julai, 2014, magazeti ya Nipashe (Toleo Na. 05781), Mtanzania (Toleo Na. 7514) na Mwananchi (Toleo Na. 5097) yaliandika makala mbalimbali kuhusu Mkataba wa Utafutaji na Ugawanaji Mapato (PSA) kati ya Serikali, TPDC na Kampuni ya Statoil ya Norway katika kitalu Na.2 kwenye Bahari Kuu.

Magazeti hayo yakiwa na vichwa vya habari tofauti kama vile “*Mapato ya Gesi Asilia Tanzania Kulizwa; Tanzania kupoteza Sh. 1.6 trilioni za Gesi na Mkataba wa Gesi wavuja*” kwa makusudi au kwa kutoelewa yalitoa taarifa za kupotosha umma kuhusu Mkataba huo. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linapenda kuwafahamisha wananchi kuwa taarifa hizo **siyo sahihi, za upotoshaji, hazijafanyiwa utafiti na uchambuzi wa kina** na zilitolewa bila uelewa wa kutosha kuhusu shughuli za utafutaji mafuta. TPDC inapenda kutoa ufafanuzi wa taarifa hiyo kama ifuatavyo.

Ufafanuzi

Baada ya Duru ya tatu ya Zabuni ya kunadi vitalu kukamilika Mwaka 2007, Serikali ilisaini Mkataba na Kampuni ya Statoil kwa ajili ya **kutafuta mafuta** katika kitalu Na. 2 kwenye Bahari kuu. Hii ilikuwa mara ya kwanza kufanyika utafiti katika Bahari kuu ya Afrika Mashariki (Somalia, Kenya, Tanzania na Msumbiji). Aidha, maeneo haya hayakuwa na ugunduzi wa mafuta. Kwa kuwa utafiti wa aina hiyo ulikuwa unafanyika **kwa mara ya kwanza nchini**, Kampuni ya Statoil ilipendekeza kwenye zabuni yake

kuwa, ikiwa itagundua mafuta ipewe **asilimia 95** ya mgawo wa faida na Serikali asilimia 5 kwa ngazi ya kwanza (*first tranche*). Chini ya utaratibu wa utafutaji mafuta, Kampuni hiyo inatakiwa kulipia gharama zote za utafiti na kubeba *risks* zote za kutafuta mafuta kwenye Bahari kuu. Utaratibu huo pia unaainisha kuwa kama hakitagundulika kitu chochote, **Serikali haitawajibika kuirudishia** Kampuni hiyo gharama ilizotumia katika utafiti huo.

Baada ya majadiliano ya kitaalamu na kina na kulingana na mazingira yaliyokuwepo wakati ule, Serikali kupitia Kamati ya Majadiliano (GNT) na kwa kutumia Mkataba wa mfano uliokuwepo wakati ule (*Model Production Sharing Agreement – MPSA, 2004*) makubaliano yalifikiwa kwamba, ikiwa mafuta yatagunduliwa, Kampuni ya Statoil itapata **asilimia 70** kama gawiwo la faida na Serikali **asilimia 30** kwa ngazi ya kwanza na kwamba Kampuni italipa kodi asilimia 30% kutoka kwenye gawio lake. Gawio hilo la faida kwa Serikali halihusishi mapato yatokanayo na ulipaji wa mrahaba – *Royalty (asilimia 5)*, gawiwo kutokana na ushiriki wa TPDC – *Participating interest (asilimia 10)*, na ushuru wa huduma – *Service levy (asilimia 0.3)*. Aidha, Serikali itapata pia kodi kutokana na gawio la Kampuni kwa kiasi cha asilimia 30. Mapato haya yote yanalipwa pasipo Serikali kutakiwa kuwekeza fedha zozote katika shughuli husika. Uchambuzi uliofanywa na Serikali na vyombo mbali mbali vya Kimataifa ni kwamba mkataba huu wa Statoil utalipatia Taifa gawio la **asilimia zaidi ya 61** na Kampuni yenyewe **asilimia 39**. Hivyo, si kweli kwamba Tanzania italizwa na kupoteza Sh. 1.6 trilioni kama ambavyo magazeti husika yalivyotaka kuupotosha umma wa Watanzania.

Aidha, nyongeza ya Mkataba (*Gas Addendum*) iliyosainiwa Mwaka 2012 kati ya Serikali na Statoil ilitokana na Mkataba wa Awali kuwa ulihusu shughuli za **Utafutaji na Ugawanaji wa Mapato ya Mafuta**. Hata hivyo, kwenye Mkataba huo kuna kipengele kinachoelekeza kuwa ikiwa gesi asilia itagundulika badala ya mafuta, basi pande mbili katika Mkataba husika zitajadiliana kuhusu namna ya kuendeleza gesi asilia itayogundulika ikiwemo uthaminishwaji wa gesi asilia, viwango vya uzalishaji na ugawanaji mapato, na ujenzi

wa miundombinu ya kufikisha gesi asilia kwenye soko la ndani na nje.

Bila kusainiwa kwa Mkataba katika Kitalu Na. 2 kwenye Bahari kuu katika ya Serikali na Statoil Mwaka, 2007 ugunduzi mkubwa wa gesi asilia ambao kwa sasa umefikia takriban **futi za ujazo trilioni 50.5** usingefanyika. Aidha, kusainiwa kwa mkataba huo kumefungua maeneo mapya ya utafutaji mafuta, kumewezesha kupatikana kwa takwimu za kitaalamu ambazo hapo awali hazikuwepo, kumeiingiza Tanzania kwenye ramani ya dunia katika masuala ya utafutaji mafuta na kuharakisha maendeleo ya utafutaji mafuta na gesi asilia.

Hitimisho

Serikali kupitia TPDC itaendelea kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika shughuli za utafutaji mafuta kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha Mikataba ya Utafutaji na Ugawanaji Mapato ili iendane na mazingira yaliyopo. Mwisho napenda **kuviasa vyombo vya habari na wenye tovuti za kijamii kuzingatia misingi na miiko ya uandishi wa habari** kwa kutoupotosha umma kwenye masuala ya msingi kuhusu mustakabali wa nchi yao.

TPDC itaendelea kutoa elimu kuhusu tasnia ya mafuta na gesi asilia na Shirika liko tayari wakati wowote kutoa maelezo ya kina kwa mwananchi yeyote mwenye lengo la kutaka kuielewa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini.

Imetolewa
Mkurugenzi Mtendaji
TPDC